MAOMBI YA FAMILIA



DENIS & DEVIS
JULIUS

MAOMBI MAALUMU KWA AJILI YA FAMILIA ZETU

~Kanisa la nuru ya upendo wa Kristo

Huu ni mwongozo wa maeneo muhimu ambayo unapaswa uyagusie katika kuiombea familia yako.

Familia yaweza kuwa walio katika ndoa yako, yaani mume/mke, na watoto, au yaweza kuwa baba, mama, kaka, dada, au yaweza kuwa ndugu wa mbali kama vile mjomba, shangazi, binamu, shemeji n.k. makundi yote haya ambayo yanamahusiano na wewe. kiroho ni familia yako, na hivyo hauna budi kuyaombea wewe kama mwamini, kwasababu tusipofanya hivyo hatutimizi agizo la Mungu la sisi kuwa wapatanishi.(1Samweli 12:23, 1Timotheo 5:8). Haya sio maombi ya kuomba kama ile sala ya dakika mbili ya chai asubuhi, hapana bali ni maombi yanayochukua muda, kwasababu itakugharimu uwataje mmoja mmoja uwaombee.

Maeneo yapo matano (5), ni vema kila eneo ukatumia saa moja (1). Unaweza kugawanya kila siku kipengele kimoja, au ukaenda vyote kwa pamoja ni kwa jinsi uwezavyo.

1) WOKOVU

Hili ndio eneo la kwanza na ndio la muhimu kuliko yote kuliombea. Ikiwa wewe umepokea neema ya wokovu, Mungu kukuweka hapo ndani ya hiyo familia ni ili ujenge palipobomoka. Hivyo ni kuwaombea watu wako sikuzote bila kuchoka wala kukata tamaa, maadamu wapo hai, usiache kuwaombea wokovu wa kweli juu yao. Kuna mtu anasema nimemwombea mume wangu kwa mifungo na mikesha mingi lakini sioni dalili yoyote ya kuokoka, hivyo nimeacha. Ndugu nataka nikuambie si kazi yako kujua Mungu anatendaje kazi, tukiomba tumeambiwa tuamini, kwamba tumesikiwa na kujibiwa.

Kulikuwa na mchungaji, mwenye kijana wake ambaye suala la wokovu lilikuwa mbali naye. Hata alipojaribu mara nyingi kumuhubiria hakuvuna chochote, Lakini jambo alilolifanya Yule mchungaji hakuacha kumwombea mwanae kila siku aokoke. Aliendelea kufanya hivyo kwa miaka kadhaa mpaka alipokufa na kwa bahati mbaya wakati huo wote hakushuhudia

mwanawe kama ana dalili yoyote ya kuokoka. Lakini baadaye yule mtoto baada ya kuondokewa na baba yake, neema ya Mungu kufuatana na maombi ya baba yake ikaanza kufanya kazi ndani yake, akatubu, akampokea Yesu, lakini jambo lile halikuishia pale, yule mtoto akaja kuwa mchungaji kama baba yake na mhubiri mkubwa sana, ambaye alifanya kazi ya kuwavuta wengi kwa Kristo hata zaidi ya baba yake mzazi.

Hivyo usiipuuzie nguvu ya maombi. Hata kama una ndugu ambao tayari wameshaokoka, huna budi kuendelea kuwaombea imani yao isiharibiwe. Kwasababu adui huwa anatembea kuwapinga. Unajua Ayubu aliitwa mcha Mungu kwasababu aliamka kila siku asubuhi kuwaombea watoto wake rehema kwa Mungu. Hakujali wokovu wake peke yake, bali na wa familia yake pia,.

Katika eneo la wokovu Gusia.

- *Kuwaombea rehema.*

Ayubu 1:5
[5]Basi ilikuwa, hapo hizo siku za karamu zao zilipokuwa zimetimia, Ayubu hutuma kwao akawatakasa, kisha akaamka asubuhi na mapema, na kusongeza sadaka za kuteketezwa kama hesabu yao wote ilivyokuwa; kwani Ayubu alisema, Yumkini kwamba hawa wanangu wamefanya dhambi, na kumkufuru Mungu mioyoni mwao. Ndivyo alivyofanya Ayubu sikuzote.

- *Ombea awe na moyo wa kuikubali injili kutoka kwako.*

Wakati mwingine ugumu wa kuiamini injili yako unayowapelekea, hutokea, kisa tu wewe ni ndugu yao, hivyo waombee ugumu wa moyo usiwakute. Katika maombi haya hakikisha unamtaka mmoja mmoja.

Mathayo 13:57 Wakachukizwa naye. Yesu akawaambia, Nabii hakosi kupata heshima, isipokuwa katika nchi yake, na nyumbani mwake mwenyewe.

- *Ombea mioyo yao ichomwe waisikiapo injili mahali pengine.*

Matendo 2:37 Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu? 38 Petro akawaambia, Tubuni

mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

- *Waombee wasisongwe na masumbufu ya maisha haya, wakashindwa kumzalia Mungu matunda.*

Luka 8:14 Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote

- Waombee mani zao zisiharibike.

Kwa wale ambao tayari wameshaokoka, endelea kuwaombea juu ya imani zao, wasirudi nyuma, bali waendelee kuwa moto, siku baada ya siku. Wakue kiroho, waongezeke kimaombi, kimifungo, na kiibada.

Luka 22:32 lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako.

- *Waangaze nuru zao*

Bwana hataki wokovu wetu tuufiche mioyoni mwetu tu, bali anataka pia ujulikane kwa wengine. Waombee ujasiri wa kuudhihirisha wokovu wao kwa wengine, ili injili ya Kristo ihubiriwe pia kupitia wao, ndugu wengine kwenye familia waokoke. Wasiwepo wakina nikodemo waliookoka chini kwa chini.

Mathayo 5:16 Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.

Maombi ya wokovu na kuendelea kusimama yakazanie sana kwa ndugu zako, huku ukikumbuka hata wakipata vyote kama hawana Kristo ni ziwa la moto. Hatupendi kusikia hivyo, basi tukazane kuwaombea bila kusahau pia kuwashuhudia.

2) TUNDA LA ROHO.

Eneo la pili la kuombea katika familia ni Tunda la Roho.

Wagalatia 5:22 Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23 upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria

Familia nyingi zimepoteza hizi tunu. Utaona ndugu na ndugu hawaongei, hawapendani, hawasaidiani, wamewekeana matabaka. Ni familia moja, damu moja, lakini kila mtu yupo na maisha yake, wanatukanana, wanapigana. Wakikutana ni kwenye matukio maalumu kama misiba tu, zaidi ya hapo hamna, wanandoa wapo nyumba moja lakini kila kukicha ni malumbano..Asilimia kubwa ni adui ndiye anayeleta mafarakano haya. Hivyo hili ni eneo la pili na la muhimu pia kuliombea.

Wataje majina mmoja mmoja, ombea Mungu aweke tunu hizo mioyoni mwako, na kwenye familia nzima na ukoo mzima, hata kama utaona kuna amani, ombea amani zaidi, hata kama utaona kuna upendo, ombea upendo wa mwisho uzidi ule wa kwanza.

Gusia,

- *Bwana aweke upendo usio na unafiki ndani ya familia.*

Warumi 12:9 Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema

- *Bwana ajenge Uvumilivu.*

Migogoro mingi hususani ya kindoa inazuka kwasababu ya kukosa kuvumiliana. Adamu aliweza kumvumilia mkewe Hawa, alipokosa, na akaendelea kuishi naye hakumwacha. Mahali popote palipo na uvumilivu pana ushindi.

- *Bwana aweke amani*

Familia zinahitaji amani ya Kristo. Hata kama mtakuwa na amani, ombea amani zaidi, vita, mashindano, wivu, visasi, kuchukiana, visizuke kwenye familia, hadi ukoo wako.

- *Ombea na matunda mengine yote, kama vile uaminifu, fadhili, upole, na mengineyo yaumbike ndani ya mioyo ya familia.*

3) **AFYA**

Maradhi huathiri, ustawi wa familia. Baba akiwa mgonjwa, atashindwa kufanya kazi watoto hawataenda shule. Maradhi ni kazi ya shetani. Na tunayadhibiti kwa kuwa waombaji. Kumwambia Bwana, ulishayachukua magonjwa yetu miaka elfu mbili iliyopita hivyo hayo magonjwa hayana nafasi katika familia zetu.

Bwana alisema..

Kumbukumbu la Torati 7:15
[15]Na BWANA atakuondolea ugonjwa wote; wala hatatia juu yako maradhi yo yote mabaya uyajuayo ya Misri, lakini atayaweka juu ya wote wakuchukiao.

Gusia,

- *Magonjwa ya kurithi*

Bwana afute magonjwa yote ya kifamilia, au ya kiukoo, au kurithi katika familia yako.

- *Magonjwa sugu.*

Magonjwa yasiyotibika kwa haraka, na ya kujirudia rudia, Bwana ayafutilie mbali.

- *Madhaifu yote:*

Ulemavu katika mwili, viungo vya ndani, moyo, akili, macho n.k. havina nafasi katika nyumba yako.

4) **ULINZI:**

Mara nyingi adui hupanga uharibifu. Hivyo hatuna budi mara kwa mara kuombea ulinzi juu ya familia zetu na mali zetu, wakati wewe uwapo salama hujui ndugu yako yupo safarini, na adui ameweka mitego yake ya ajali afe, au anatembea usiku majambazi wamepanga kumvamia na kumpiga, hujui wachawi wametumwa wamuue,..Hivyo uonapo salama usidhani adui hawawindi, waombee kila siku ulinzi, wataje kimajina, mmoja

mmoja, Bwana akaizungushie wigo wake kama alivyoizungushia familia ya Ayubu.

- Ombea, wigo wa Bwana uifunike familia (Ayubu 1:10)
- Ombea malaika wa Bwana watembee na ndugu zako (2Wafalme 6:17)
- Ombea majaribu mbalimbali ya adui mfano wa yale Ayubu, yasizuke kwenye familia yako, Kama moto, majanga, ajali. (Luka 22:40)

5) **MAFANIKIO:**

Kufanikiwa kwa ndugu zako, ni kufanikiwa kwako pia na jamii pia.

- Waombee Mungu awape kazi wale ambao hawana kazi, ndani ya familia.
- waombee Mungu awape biashara wale ambao hawana biashara. Mungu awainue kimaisha, waweze kujikimu wenyewe na kuwasaidia na wengine. Kwasababu adui pia huzuia uchumi wa watu, ili tuendelee kubaki katika hali za kupungukiwa kabisa. Hivyo kumbuka jinsi uwaombeavyo ndivyo wafanikiwavyo.
- Waombee mafanikio yote pia ya kimipango, elimu, huduma, n.k. yote hayo huna budi kuyaombea kwenye familia yako.

3 Yohana 1:2
[2]Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.

Yoshua 24:15
[15.. lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA.

Bwana akubariki.

Kamwe kila siku usiache kuyaombea haya maeneo. Na Bwana ni mwaminifu atasikia na kuiponya familia yako.

MAWASILIANO:

Mch. Denis & Devis Julius
Nuru ya upendo
+255693036618 /+255789001312
info@wingulamashahidi.org
www.wingulamashahidi.org